

**MKATABA WA UPANGAJI WA CHUMBA
CHA BIASHARA.**

(kwenye Kiwanja Namba 204 Kitalu "T" Mtaa wa Lumumba, Wilaya ya
Nyamagana katika Mkoa wa Mwanza)

MKATABA HUU umefanyika hii leo tarehe⁰⁹.....
Mwezi.....⁰⁹.....2025.

KATI YA

MAULID HONEJA KAJI (kwa niaba ya **ZIPOURE PAUL BOMANI**) wa S.L.P 1069 Dar es Salaam-Tanzania (ambaye katika mkataba ataitwa "**Mpangishaji**") kwa upande mmoja.

NA

NAWADA TANZANIAN COMPANY LIMITED wa Mwanza-Tanzania mwenye namba za simu 0744664491 (ambaye katika mkataba ataitwa "**Mpangaji**") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mpangishaji ana mamlaka halali ya kupangisha kwenye jengo la biashara kwenye kiwanja Na. **204** Kitalu "**T**" Mtaa wa Lumumba, Wilaya ya Nyamagana katika Mkoa wa Mwanza.

NA KWA KUWA Mpangishaji kwa hiari yake mwenyewe ana nia na ameamua kumpangisha Mpangaji kwenye chumba cha biashara namba D9 kwenye jengo tajwa, na Mpangaji kwa hiari yake mwenyewe amekubali kupangishwa kwenye chumba hicho kwa makubaliano yaliyo ndani ya mkataba huu.

BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:-


1. **Kwamba**, Mpangishaji amepangisha Mpangaji chumba cha mbele kwenye jengo tajwa hapo juu kwa muda wa miaka miwili kuanzia tarehe 09/10/2025 mpaka tarehe 09/10/2025.
2. **Kwamba**, kodi ya chumba iliyokubaliwa na pande zote mbili kwa miaka miwili ni Fedha za Kitanzania Shilingi Milioni Nane tu (**Tshs. 8,000,000/=**).
3. **Kwamba**, siku na tarehe ya kuweka saini katika makubaliano haya Mpangaji amemlipa Mpangishaji kiasi cha fedha za Kitanzania Shilingi Milioni Nane tu (**Tshs. 8,000,000/=**), kiasi ambacho Mpangishaji anakiri kupokea.
4. **Kwamba**, Mpangaji atatumia chumba hicho kwa shughuli za biashara pekee na vile vile hataruhusiwa kumpangisha mtu mwingine bila ridhaa ya maandishi kutoka Mpangishaji.



5. **Kwamba**, kila upande unayo haki ya kusitisha mkataba huu lakini ni kwa kuupa upande mwingine taarifa ya maandishi ya nia ya kusitisha mkataba huu ya mwezi mmoja kabla ya tarehe inayokusudiwa kusitisha lakini bila kuathiri haki na wajibu wa upande wa pili wa mkataba huu.
6. **Kwamba**, taarifa hiyo ya mwezi mmoja itatumika pia pale Mpangaji atakapohitaji kuongeza mkataba wake kwa muda mwingine atawajibika kumtaarifu Mpangishaji kabla ya tarehe ya kuisha mkataba na kushindwa kufanya hivyo Mpangishaji atakuwa huru kumpangisha mtu mwingine kwenye chumba hicho baada ya kuisha mkataba.
7. **Kwamba**, gharama zote za umeme na maji na tozo mbalimbali kama zitakuwepo toka mamlaka husika kwa kipindi chote cha mkataba huu zitalipwa na Mpangaji.
8. **Kwamba**, katika kipindi chote cha mkataba huu, sheria, taratibu na kanuni zote zinazoongoza masuala ya upangaji zitazingatiwa na kwamba zitatumika ikitokea ukiukwaji mkubwa wa vipengele vilivyo ndani ya mkataba huu.


KWA USHAHIDI MKATABA HUU UMESAINIWA NA WAHUSIKA SIKU, TAREHE, MWEZI NA MWAKA KAMA IFUATAVYO.

UMESAINIWA NA KUTOLEWA na **MAULID HONEJA KAJI (kwa niaba ya ZIPURE PAUL BOMANI)** ambaye anaelewa kusoma na kuandika lugha iliyotumika katika uandaaji wa mkataba huu na ambaye namfahamu binafsi/ ametambulishwa kwangu na.....
leo tarehe ...09... mwezi.....10.....2025.


.....
MPANGISHAJI

MBELE YANGU:

Jina: JACKSON BARNABAS MALINDABU

Sahihi: 

Anuani: 10193, KWAHARA

Wadhifa: WAKILI



UMETAJIWA NA KUTOLEWA na
Namulanda Daniel
Kwa niaba ya **NAWADA TANZANIAN
COMPANY LIMITED**
ambaye anaelewa kusoma na kuandika
lugha iliyotumika katika uandaaji wa
mkataba huu na ambaye namfahamu
binafsi/ ametambulishwa kwangu
na Mtulia E.O.
leo tarehe 09 mwezi 10 2025.


MPANGAJI

MBELE YANGU:

Jina: Jackson Barzabas Maliyabey

Sahihi: 

Anuani: 10173, Mwanzi

Wadhifa: Wakil



Mkataba huu umetayarishwa na:
Pande Mbili za mkataba huu.